



## **CHUO CHA ARDHI MOROGORO**

### **RISALA YA MKUU WA CHUO KUKARIBISHA WANACHUO 2018/2019**

**TAREHE 06/11/2018**

**Mkuu wa Taaluma,**

**Mkuu wa Utawala,**

**Mshauri wa wanachuo,**

**Wakufunzi,**

**Wafanyakazi wenzangu,**

**Rais wa chama cha wanachu ARISO,**

**Wanachuo,**

Jina langu ni **Adam Nyaruhuma**, Mkuu wa Chuo

Leo nina furaha kubwa.

Tumefungua Chuo cha Ardhi kipya chenye wanachuo zaidi ya 350.

Mwaka huu pamoja na wanachuo wa kozi za siku nyingi za Geomatikia tumeanzisha kozi mpya za Mipango Miji na Vijiji.

Nawakaribisha sana wanachuo wanoendelea na masomo katika Geomatikia na wanachuo wapya wa Geomatikia na Mipango Miji na Vijiji.

Wanachuo wetu wapya wa URP, upungufu utakao jitokeza tutaurekebisha. Tupeni ushirikiano. Hongereni kwa kuwa wa kwanza kweye kozi hii. Kazi kubwa imefanyika kukipanua na kukiendeleza japo haijakamilika.

Wanachuo mnaoendelea, najua mmefurahi chuo chetu kupanuka, tunawaomba mvumilie mauzi madogomadogo yatakayojitokeza katika kutumia kwa pamoja raslimali kama mabweni nk. Wanachuo wetu wapya wa URP tuwapokee na kutengeneza jumuiya moja ya ARIMO.

Wakufunzi na wafanyakazi wenzangu, viongozi wa ARISO na wanachuo wote tujitahidi ili kuongezeka kwa wanachuo kuende sambamba na ubora wa elimu na mazingira ya chuo.

Wanafunzi, mjifunze kwa bidii rasilimali tunazotumia zisipotee bure. Taifa linawategemea.

Nawashauri pia, kila atakayefanya udanganyifu wa mitihani tutamuondoa chuoni mara moja.

Maisha ya ARIMO mara ya kwanza yanaweza kuwa tofauti na wanachuo wengi walivyozea. Hakuna kuvalaa uniformu na hakuna kupangiwa pa kwenda au wakati wa kwenda na kurudi. Hii ni fursa lakini ikitumika vizuri.

Wanachuo wote tumewaandalia mabweni, vitanda na magodoro. Wanaopenda kukaa nyumbani pia wanaruhusiwa.

Kama kukiwa na tatizo lolote eleza uongozi wa chuo kama Mshauri wa Wanachuo, Mkuu wa taaluma, Mkuu wa chuo.

Chuo chetu kinasifika kwa ubora wa wataalamu tuna ozalisha na huduma tunazotoa kwenye miradi

Natumaini kila mmoja atajitahidi tuendeleza ubora na sifa hii.

Nawatakia kila la kheri.